

Taarifa ya gharama Nyumbani

Karatasi la uhakika wa muongozo wa pesa zako



Taarifa ya gharama ni nini?

Taarifa ya gharama ni mpango uliyoandikwa ili kukusaidia wewe kudhibitisha kiasi cha pesa zinazolingia kama mapato na idadi ya matumizi yako. Hi ni muhimu kukusaidia wewe kufuatilia vitu unavyogharamia.

Nini kilicho katika taarifa ya gharama?

- ▶ Mapato yako – pesa ngapi unaingiza na wapi zinakotoka (kwa mfano, mishahara au kutoka Centrelink).
- ▶ Matumizi yako – pesa ngapi unazotumia na wapi unapozitumia pesa (kwa mfano, kwenye bili, chakula na karo ya shule).

Taarifa ya gharama humaanisha unaweza:

- ▶ kuweka usahihishi wa kawaida kwenye pesa zinakoenda
- ▶ kulipia vitu unazohitaji kama chakula na bili za sasa
- ▶ kujitayarisha kwa hali ya ghafla na matumizi yasiyopangiwa
- ▶ kuweka akiba kwa ajili ya kitu maalumu
- ▶ kuamua kama jamii jinsi ya kutumia pesa zako

Kumbuka

- ▶ Taarifa ya gharama ni mpango uliyoandikwa ambao unakusaidia wewe kujua pesa ngapi zinazolingiangapi zinazolingia (mapato) na nini unahitajika kuzitumia kwake.
- ▶ Taarifa ya gharama hukusaidia kugundua matumizi yako
- ▶ Kwa taarifa ya gharama kutimizwa ni lazima kuifuatilia.

Mahali pa kupata usaidizi na maelezo zaidi

Kama ukiwa na shida za pesa, wasiliana na Mshauri wa Kifedha bila malipo kwenye simu 1800 007 007.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Mshauri wa Kifedha, au kukamilisha hati ya mpango wa taarifa ya gharama kwenye tuvuti, tembelea tuvuti ya MoneySmart, www.moneysmart.gov.au, au pigia Afisa wa Huduma ya Maelezo ya Kifedha kutoka Centrelink kwenye simu 13 23 00 ili kupata usaidizi jinsi ya kupanga bajeti yako.

Kufanya taarifa ya gharama kukufanyia kazi wewe

Atem na Arop hawana taarifa ya gharama kwa wakati wanaponunua kwenye duka kuu. Wanaandika nini kinachohitajika kuwa kwenye orodha ya kununua lakini wanapofika kwenye duka kuu haichukui muda mrefu kabla ya kuanza kubishana kuhusu nini kununua. Arop anataka kununua pekee kilicho kwenye orodha lakini Atem kila mara anataka kununua chakula zaidi na mara nyingine vitu wasivyohitaji, kama tafrija.

Siku moja walipoenda kununua, Atem aliweka vitu kadhaa kwenye toroli ambazo hazikuwa kwenye orodha kwa sababu zilikuwa kwenye seli. Wakati walipokuwa wanafaa kulipa, walijumlisha \$70 na Arop alikuwa na \$30 pekee. Alipata aibu na ilimbidi kuwacha nyuma vyakula zaidi kwenye duka kuu kwa sababu hakuwa na pesa za kutosha.

Baada ya kujadiliana mawazo, Atem na Arop waliamua kujitayarisha ili kujua pesa ngapi wanaweza kutumia ndani ya juma moja katika duka kuu. Waliamua kuiweka taarifa ya gharama. Walifanya hivi na wakati waliponunua chakula hawakuaibika tena kwa kuwa na zaidi kwenye toroli kuliko wanavyoweza kutosheleza ili kulipia.

This page has been intentionally left blank.